# WE′ KUWEZA?

**© Muddyb Mwanaharakati**

Kimechapishwa na,
Dar Genera Publishing,
Dar es Salaam,
Tanzania.

Mhariri: Dickson Mtalaze
Jalada: Frank Masai

© Muddyb Mwanaharakati, 2021
Mobile: 0713-538-427

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kinakili, kutafsiri, kupiga chapa au kukitoa kitabu hiki au sehemu yake kwa njia yoyote ile bila idhini ya Muddyb Mwanaharakati.

Chapa ya Kwanza 2021

**ISBN**: **978-9976-5467-6-7**

## SHUKRANI

Shukrani jazilan kwa Mola wetu mtukufu, muumba ardhi na mbingu kwa kuniongeza pumzi nyingine niliyoitumia katika kuhakikisha kitabu hiki kinamilika. Lilikuwa wazo moja lililoning'inia akilini tangu Julai 2020, mapema mwaka 2021 nilianza kutoa madini kichwani na kuyaweka katika karatasi.

Ninapenda kuwashukuru wale wote walionisaidia katika mambo ya kisheria, hasa Mariam Mbano—ulikuwa wa kwanza kunifungua kisha nikaendelea mbele zaidi hadi katika baadhi ya mitandao, hasa Bongo 5, EATV na wavuti ya magereza Tanzania. Haikuwa rahisi sana kuelezea mambo ya kisheria lakini nililazimika kurejea maelezo hayo ili kuleta uhalisia wa mambo husika.

Tatu, ningependa nimshukuru mdogo wangu Dickson Mtalaze kwa kunyoosha lugha katika riwaya hii na kunikumbusha juu ya mambo mbalimbali niliyokuwa sijayaona kabla yake. Unisamehe kwa kuingilia ratiba zako lakini mkono wako kuwamo humu umezidi kufanya kitabu hiki kizidi kunoga. Sijutii kukupatia kwa kweli. Shukrani sana!

Mwisho kabisa ningependa kuwashukuru wasomaji wangu kindakindaki; Jamila Kimoto, Hellen Chris, Winfrida Magawa, Mussa Simba, Godfrey Makaranga, Buinda Mjungu, Salim Al Jabry, Kefa Mkombola, Adam Mustaafrika, Khalid Gugu, Salvius Tibenda, Idrissa Abdallah na Kondo Zahran.

Shukrani za mwisho ziwaendee wanachama wenzangu wa READING MARATHON. Ahsante sana. Ninawapenda.

Mohamed Lupinga (Muddyb)
Chanika, Dar es Salaam,
9 Februari, 2021—Jumanne.
Saa kumi na mbili dakika 51 jioni.

# WE' KUWEZA?

## MLANGO WA KWANZA

Nje ya Gereza la Ukonga, 10 Disemba 2018—Dar es Salaam

MWANAMAMA mwenye umri kati ya miaka arobaini hadi arobaini na tano, alitoka gerezani na kusimama nje ya jengo la gereza kwa muda wa dakika kumi. Alikuwa akitalii kila kile ambacho hakuwahi kukiona hapo awali. Alivyoingia, sivyo alivyotoka. Akatazama pande zote pengine kutakuwa na nduguze wamekuja kumpokea, hapakuwa na mtu. Hilo halikuwa kubwa kwake kupita uhuru wake aliokuwa akiuomba kila afumbuapo macho akiwa kamili na uzima wake.

Aliamini iko siku isiyo na jina atakuwa huru. Siku yenyewe ndiyo hii. Akaanza kushikwa na huzuni, akajisogeza hadi kando ya lango kuu la gereza, akaketi. Akainua khanga yake na kujifuta machozi. Getini kulikuwa na askari aliendelea kumwangalia kila alipopiga hatua. Akageuka tena nyuma kuangalia kuta kubwa kuukuu za gereza jinsi zinavyoonekana kwa nje. Leo hii anaweza kufanya chochote bila masharti yoyote yale. Chozi tena likatoka.

"Ahsante Mungu! Sijui kipi kikubwa nilichotenda kwako hata leo hii mimi kuwa mtu huru!" mama huyo alisema akinyoosha mikono juu. Yule askari magereza aliyekuwa akimtazama kwa muda akatoka na kusogea hadi pale alipo yule mama. Akasimama mbele yake, mama hakushtuka tena. Keshawazoea. Miaka kumi ndani ya jumba moja usiloona nje, makofi, masingi, manyanyaso yasiyo na mfano, yote hakuna jipya kwake. Alijua hata akimtesa leo, itakuwa ndiyo mwisho wake kumfanyia stihizai zile atakazo.

"Mama!" askari magereza alimuita akasita kwa nukta chache. Mama mwenye kububujikwa na machozi akainua kichwa chake kumtazama askari huyo. "Naam, baba!" mama aliitika kwa kilio chenye

mseto wa furaha. "Nakusikiliza!" aliongeza. Askari akamsogelea zaidi. Akainama kiasi na kumshika bega la mkono wa kushoto wa mama huyo kwa mkono wake wa kulia, akasema. "Umepata msamaha wa rais uliotangazwa jana. Hivyo basi huna haja ya kubaki hapa. Nafikiri unawaza kuhusu nduguzo, sidhani kama kuna mwenye taarifa. Tambua tu, hii ni kama *surprise* kwako, amini kilichokutokea!" askari akanyamaza kidogo. Akaendelea; "Nauli umepatiwa, rudi nyumbani ukapumzike. Wahi ukaione familia yako. Fikiria kuanza maisha mapya. Ujitahidi usirudi tena humu. Si kuzuri hata kidogo! Kwa kusema hayo, sasa naomba uinuke, wende zako," askari alihitimisha.

Mama hakubisha agizo la askari. Akainuka polepole, akakung'uta uchafu kiasi ulioganda katika khanga yake, akaianza safari. Hakumaliza hata eneo la magereza, akarudi tena nyuma kwa yule askari. "Naam, mama!" askari alisema baada ya kumuona mama yule akirudi kwa shauku.

"Nini hasa nilichokifanya hata nikapata msamaha huu?" mama huyo aliuliza. Askari akameza funda la mate kiasi huku akimkata jicho la huruma, akasema; "Sina vitu vingi vya kisheria ninavyoweza kukuelezea ili utambue msamaha wako umetokeaje. Ila nitajaribu kueleza kwa kadiri nitakavyoweza kuilezea '*parole*' namna inavyofanya kazi," akageuka nyuma kutazama askari wenzake. Akaendelea, "*Parole* ni utaratibu wa kisheria unaompa fursa mfungwa aliyehukumiwa kutumikia kifungo gerezani cha miaka minne na kuendelea kutumikia sehemu ya kifungo chake katika jamii kwa masharti maalum baada ya kukidhi vigezo vifuatavyo, mosi; awe ametumikia theluthi (1/3) ya kifungo chake na kuonesha mwenendo wa kurekebika kurudi katika jamii kumalizia sehemu ya kifungo chake kwa masharti maalum.

Ikiwa ni pamoja na kuwa chini ya uangalizi maalum kuhakikisha hatendi kosa lolote hadi hapo atakapomaliza sehemu ya kifungo chake. Kuzingatia masharti ya *parole* anayopewa kikamilifu,

kuwa raia mwema na kuishi kwa kujipatia kipato halali katika jamii. Pili, Awe ameonesha kujutia kosa, kurekebika tabia na kuonesha mwenendo mzuri gerezani, mamlaka husika kujiridhisha kuwa hatahatarisha usalama wa jamii. Wanaostahili na huduma ya *parole* ni kama ifuatavyo, mosi, asiwe amehukumiwa kifungo cha maisha, asiwe mfungwa anayetumikia kifungo kwa makosa ya unyang'anyi wa kutumia silaha, madawa ya kulevya na makosa yanayohusiana na kujamiiana, asiwe mfungwa ambaye kifungo chake kimebatilishwa kutoka kwenye kifungo cha kunyongwa, awe anatumikia kifungo kisichopungua miaka minne (4) au zaidi na awe ametumikia 1/3 ya kifungo chake, awe ameonesha tabia na mwenendo mzuri kwa muda wote aliokaa gerezani, asiwe na pingamizi la kimahakama la kukataliwa kunufaika na utaratibu wa parole chini ya kifungu cha 67 cha sheria ya makosa ya jinai.

Kimsingi *parole* inahusisha jamii katika suala zima la urekebishaji wa wafungwa badala ya kutegemea serikali peke yake kwani chanzo cha uhalifu ni mazingira yanayotokana na jamii yenyewe. Je, ulihukumiwa miaka mingapi?"

"Miaka thelathini!" mama huyo alijibu.

"Umekaa miaka mingapi ndani?"

"Tangu 2008!"

"Basi upo katika orodha ya wanufaika," askari huyo alijibu huku akimtazama kwa umakini mkubwa mama huyo. "Haya sasa mama nenda nyumbani ukapumzike. Iwahi familia yako!" akaongeza akitoa tabasamu hafifu.

Akachanganya miguu kwa furaha mbio hadi ng'ambo ya barabara. Akasogea hadi eneo la kituo cha daladala, akaungana na raia wengine walio huru, kwa furaha aliyonayo, hakuona tabu kusubiria gari kwa muda mrefu. Bado alitamani kuendelea kusimama pale kituoni akitazama nyumba mpya za maafisa wa magereza zilizojengwa upande

wa kulia kuelekea Ukonga Madafu. Hapo awali hazikuwapo. Eneo kubwa llikuwa viwanja vitupu na baadhi nyumba za kizamani. Ametoka, akakuta nyumba hizo zimeota tena zenye mwonekano mzuri kabisa.

"Kweli miaka kumi sio mchezo! Mabadiliko ni mengi mno!" alijisemea nafsini. Kabla ya tabasamu kuisha usoni pake, gari ilisimama mbele ya kituo ikitangaza eneo analokwenda.

*Ya Ubungo-Ubungo mawasiliano hiyo!*
*Ya Ubungo-Ubungo mawasiliano!*
*Chap kwa haraka kama unaenda!*
*Panda twende kama unaenda!*

Akajitoma ndani ya gari *upesiupesi*, akaketi kiti cha nyuma upande wa kulia dirishani kabisa. Kwa uchovu, akajiegemeza kichwa angalau kushangilia uhuru wake. Gari ikiwa mwendoni, na yeye akaamua kusafiri zake kimawazo. Akakumbuka namna alivyoingia jangani hata kupelekea kutumia kifungo hadi kutoka. "Sijui wanangu watanikumbuka? Lakini watanikumbuka tu!" mama huyo alijisemea nafsini. Jicho nje ya gari akiangalia mapinduzi makubwa ya nchi ndani ya miaka kumi. Akatazama mtu aliyeketi kando yake, hakuwa na habari.

Akatoa tabasamu hafifu. Ana kiu ya kumwuliza maswali mawili matatu lakini kuna sauti inamwambia *'humjui hakujui, ya nini kuumizana makoo kwa maswali!'* Akapotezea hilo. Bado mihemo na shibe ya furaha iliendelea kuutambaa moyo wake kwa majivuno makubwa. "Nikifika nyumbani, sitapika chakula chochote zaidi nitachukua familia yangu na kwenda kula nayo chakula cha jioni sehemu mahsusi!" aliendelea kuwaza nafsini. Akatoa tena tabasamu hafifu. Akamwangalia wa kando yake kama kamwona, ni kweli alimwona.

"Samahani sana! Leo nd'o nimetoka jela baada ya miaka kumi ya kifungo!" hatimaye alifunguka kile kilichomfunga kauli kwa muda

akitamani azungumze na mtu. "Aaaiii, jamani, pole sana, dada!" dada wa kando alimjibu mama huyo. Usowe ukasawijika kwa kitendo hicho. Pengine hakutegemea kama angekutana na mtu aliyetoka kutumikia kifungo halafu tena leo hii yupo uraiani kwenda kuitazama familia yake, ndugu jamaa na marafiki. "Ahsante, mdogo'angu. Nd'o maisha yalivyo!" mama huyo alijibu huku akibubujikwa na machozi. Moyo wake sasa unaelekea kuwa na ahueni.

"Ninataka kusema mengi lakini najionea shida. Nisingependa nikutwishe mizigo isiyokuhusu—nivumilie tu mdogo'angu!" aliongeza akifuta machozi kwa khanga yake. Binti wa kando akaingiza mkono katika pochi yake ndogo rangi nyeusi yenye vifungo vya rangi ya fedha, akatoa leso yake na kumkabidhi mama huyo. "Jifute na hii, tafadhali!"

Kwa unyonge, akaipokea. Akaanza kujifuta huku akivuta mafua ndani. Binti aliendelea kumsaili mama huyo aliyechoka kimwonekano, akataka kusema neno, akatulia. Akamgeukia, "Nini hasa kilitokea?" binti alihoji akimtazama usoni. Mama akainua kichwa chake na kumtazama binti aliyeuliza swali lake. Akamjibu; "Ni kisa kirefu. Pengine kama tutakutana siku nyingine n'takueleza!" mama alihitimisha kauli yake akijitupa tena katika kioo cha dirisha kwa kuegemeza kichwa chake.

Upepo wa uhuru uliendelea kumcharaza hadi kituo cha daladala cha Tabata Matumbi. Akiwa anakaribia mlangoni mwa daladala, akaingiza mkono katika kipochi chake kidogo ili kutoa pesa ya kulipia nauli; "Acha tu n'tampa mimi!" yule binti alidakia kabla mama huyo kutoa nauli yake. "Mungu akutangulie mama'ngu!" binti aliongeza. "Ahsante. Nawe pia Mungu akuzidishie ulipotoa!" alishukuru akishuka garini.

Upande alioshukia, ndiyo huohuo alioelekea taratibu hakuwa na haraka yoyote ile. Bado ushamba wa mabadiliko uliendelea kumtafuna. Ameshangaa mno kukutana na aina mpya ya taa barabarani, daraja la

Mfugale, lami iliyoboreshwa, nyumba zilizoota eneo la kwake, basi kuchanganyikiwa tupu. Alijitahidi kuingia ndani kiasi kutokea barabarani, alifika katika mji wake. Hakuiishi kwa muda wa miaka kumi. Hakuona wanawe, ndugu jamaa wala marafiki. Kawia ufike, na kweli kwa kukawia, alifika nyumbani kwake. Bahati isivyo upande wake, nyumba yake haikupitia mabadiliko yoyote yale tangu alivyoiacha.

Akapandwa na furaha ya ghafla.

"Hatimaye nimefika nyumbani kwangu!"

Ni baada ya kupita chochoro nyingi mno, nyumba zimeshonana, ujenzi ule wa bila mpangilio. Ukifanya mchezo kama huna mwenyeji, basi waweza kutokea uani kwa mtu. Pamoja na kupata tabu ya njia nyingi kufungwa kutokana na ujenzi uliotokea katika kipindi alichokuwa hayupo, bado mtu ni kwao. Nyumba yake ilikuwa na kibaraza kidogo cha zege juu. Juu yake kuna ruva za matobotobo, mbele yake kuna kuta yenye ruva pia, akajiketisha katika mkeka uliokuwa nje.

"Angalau utaratibu wa kuweka mkeka kibarazani bado ungali upo!" alijisemea nafsini akitabasamu. Akashusha pumzi akijigemeza ukutani. Hakutaka pupa ya kuingia ndani. Alijua keshafika kwake. Nini papara hata akimbilie ndani. "Niangalie ya dunia kwanza kabla ya kwenda kufakamia furaha mpya ya uhuru wangu!" alisema, akacheka tena. Safari hii cheko lilitoka na sauti kabisa. Punde akasikia mlango unafunguliwa. Akageuka kutazama aliyefungua mlango.

Banati m'bichi kabisa alisimama mlangoni kwake akimsaili aliyeketi mkekani kwake bila taarifa yoyote ile. Binti huyo alituma salamu za kichunguzi katika mwili wa mama huyo kuanzia unyayoni mpaka kisogoni. Hakubakisha hata mahali. Akasema; "Nikusaidie nini na wewe ni nani uliyekuja kuketi katika mkeka wangu bila taarifa?" usowe ulisema kama hakutania hata kauli moja. Mama mwenye nyumba hakuwa na wasiwasi, badala yake aliendelea kutabasamu tu.

Akasimama kumsikiliza huyo mwenye kujinadi kuwa yeye ndiye mwenye nyumba.

"Wanangu wako wapi?" lilikuwa swali lake la kwanza kumwuliza binti aliyesimama kizingitini kwake. "Watoto?" binti aliuliza kimshangao. "Watoto gani?" akaongeza. Sura yake ilionesha kutokuwa na habari yoyote ile kuhusu watoto. Akajieneza vilivyo hasa kizingitini akajaa. "Sema shida yako, naona unazunguka tu!" mambo yameiva. Mama huyo akashtuka kiasi. Akajitahidi kuchungulia ndani kwa namna ambayo aliona inatosha, akakuta makochi yake yako vilevile, zaidi yaliongezewa mapambo ya vitambaa. Rangi ya nyumba, wavu za dirisha, kabati la vyombo na sehemu kubwa ya sebule haikupitia mabadiliko.

"Hapa nd'o kwangu," alijisemea nafsini akimtazama yule binti aliyemkinga asiingie ndani. Akili ya haraka ikamjia, akatumia nguvu kumsukuma yule binti, akafanikiwa kuingia sebuleni kabisa. Ile picha ya mumewe akiwa katika shati rangi ya maziwa iliendelea kuning'inia katika kiambaza cha sebule, picha za watoto pia, kasoro yake yeye ndiyo imetolewa. Akaketi katika kochi zake akiishiwa nguvu.

"We' ni nani mbona unaingia kama kwako humu ndani?" yule binti sasa subira ilimshinda. Alianza kupayuka wayuwayu. Alifika hadi alipoketi yule mama. Akakunja khanga yake kibwebwe tayari kwa ugomvi. "Mimi ndiye mwenye nyumba. Hii nyumba nimejenga mimi na wale ni wanangu," akatulia kidogo akitazama presha ya binti huyo. Bado hakuelewa kibwebwe kimefungwa kwa minajili ipi.

"Toka nje!" binti alisema akirusha kofi usoni kwa yule mama. Lilimfikia pasi kuwa na habari, mkono shavuni. "Imekuwaje tena?" mama aliuliza kwa mshangao. "Tokaaa!" binti alijibu kwa teke lililotua katika mbavu za mama huyo aliyekuwa kadhoofu hali kutokana na shida na chakula duni alichokuwa akipata gerezani. Hakuweza kuhimili vishindo, akaenda chini. Binti hakutaka kupoteza muda,

akaongeza na ngumi kali iliyotua shavuni. Jino chini likisindikizwa na madonge ya damu yaliyosafiri hadi juu ya zulia jepesi lenye marembo ya marumaru ya mbao. Ikatua vyema na kuacha doa jekundu.

"We' binti una wazimu eh?" mama alifoka akiinuka kutoka pale chini alipoenda bila kutarajia. "Hata kunisikiliza hutaki unafikia hatua ya kunipiga tu?" wakati mama huyo akijaribu kujieleza, binti ari ya kutaka kuendeleza kipigo ilizidi kuchemka maungoni mwake. Akamwacha mama wa watu akiendelea kujitafakari kwa kile kilichomkuta, akaenda chumbani kuchukua hicho alichokusudia kukichukua. Punde alirudi akiwa na mkanda mkononi. Kabla mama kuchukua maamuzi sahihi ya kuepusha shari kutoka ndani ya mji huo anaodai kuwa ni wake, alishtukia tena mkanda ukitua kichwani kwake na sehemu nyingine za mwili mfululizo.

"Toka! Toka! Tokaaaa!" binti alipiga mikanda mingi mfululizo huku mama akijaribu kuzuia isimpate usoni mwake, haikusaidia. Ilitua kila alipoona binti inafaa kupiga. Alipiga kwa mtindo wa kumsindikiza atoke nje. Kutahamaki, mama yuko nje akiwa na zawadi kuu ya majeraha mikononi na baadhi ya sehemu ya kichwani. Jasho linatoka, akili imevurugika, hajui nini cha kufanya.

"Dunia, mbona umenipokea vibaya hivyo? Kwa kipigo hiki, hata jela sikuwahi kukipata. Sasa si…" akakata kauli yake kabla ya kuendelea kuilaani dunia iliyo huru. Kichuma cha mkanda kilimletea madhila makubwa. Akageuka nyuma kutazama majirani zake, hakukuwapo hata mmoja anayemfahamu. Miaka kumi kumetokea mengi mno. Sura nyingi aliziona ngeni. Kitu ambacho awali hakuchunguza mabadiliko ya mtaani kwake. Katika kutazama huko, akaona nyumba moja ya mama mwuza samaki aliyekuwa akimletea katika biashara zake ikiwa imebaki kama ilivyo, akiwa na maumivu makali, akaisogelea ile nyumba. Huko nyuma binti aliendelea kutoa matusi ya nguoni na vitisho mbali asisogee tena katika mji wake.

Mwendo tena ulimtupa mkono, alivyopigwa na kwenda chini, mguu ukashtuka. Fauka ya kutembea kwa shida, akilini mwake kuliingiwa na mdudu mpya kabisa.

Majuto!

"Heri ningebaki ndani tu. Lakini siku ya kwanza na ngeu kutoka kwa mtoto ambaye ninaweza kumzaa kabisa tena nikiwa nimekaa chini—hiyo ni dharau ya hali ya juu!" alijisemea kwa hasira akiisogelea nyumba ya mama mwuza samaki. "Hodi humu ndani!" alibisha hodi akichechemea. Akatoka msichana mwenye umri kati ya miaka ishirini na sita hadi tisa hivi. Hodi ilikuwa kubwa sana kiasi hata hakujiandaa kuja kuipokea. Alitoka akiwa na khanga iliofungwafungwa ovyo kifuani kwake, kiblauzi hakijarekebishwa vizuri, nywele timtimu. Akastaajabu kumuona mtu akiwa ametapakaa damu usoni hadi mikononi.

Nguo zimenyorodoka! Hamaki ikamshika!

"Vipi tena, mama?" msichana huyo aliuliza kwa kihoro. Jicho lilimtoka pima. "Umeshambuliwa na vibaka ama?" msichana aliongeza huku akiifikia hatua yake kwa mguu wake wa kuume. Akashuka ngazi mbili zilizokuwapo katika nyumba hiyo ya mama mwuza samaki. Akaketi katika ngazi ya mwisho kabisa miguu yake ikigusa mchanga.

"Bora ingekuwa wezi, mwanangu!" mama alisema akitoa upepo mwingi mdomoni. "Uwiii! Dunia nipumzishe basi!" mama aliongeza. Hana pa kuketi, alibaki wima akipinda mithili ya gari iliyovunja bolti ya kati. "Nimepigwa na msichana niliyemkuta katika nyumba niliyoijenga mwenyewe. Yaani, nimepigwa ndani ya nyumba yangu na mtu nisiyemfahamu!" mama huyo aliongea kwa masikitiko. Sura yake ilisawijika mno. Alianza kuiona huru yake kuwa ndiyo mateso zaidi kuliko alivyokuwa ndani ya gerezani. "Oh, pole sana, mama!" binti alisema akatulia kidogo. "Nikusaidie nini sasa?" akaongeza.

"Nina shida na mama mwuza samaki!"

"Hayupo kenda feri!"

"Wanawe?"

"Wameolewa wote hawapo!"

"We' ni nani?"

"Mi' mpangaji wake!"

"Mumewe yupo?"

"Kaenda mihangaikoni kwake…" binti akatulia tena kidogo akimsaili mama huyo mwenye zigo kubwa la dhiki asubuhi yote. "Sisi sote wapangaji tuliobakia… pole sana!" binti alimaliza kauli yake. Mama akawa hana la kuongeza. Akajizoazoa na kuianza safari ya kurudi kwao. Akatazama mkononi pochi yake ilikuwa haipo. Kumbe aliiacha ndani wakati wa purukushani. Akafikiria kuirudia pochi yake pekee aliyokuwa nayo tangu siku ya hukumu yake miaka kumi iliyopita.

Akiwa anakaribia kufika, binti akatoka nje upesi. Kumbe alikuwa akimchangulia kupitia dirishani kwake. Akasimama katikati ya mlango akasema; "Unasemaje tena we' afriti mkubwa?" binti alitanguliza maneno makali ya kukarahisha nafsi huku akishika kiuno. Akatoa maneno mengi yenye kudhalilisha utu wa mwanamke huyo. "Nimesahau pochi yangu humo ndani unamodai kuwa ni mwako!" hatimaye alisema kusudio lake. "Huna pochi humu ndani!" binti alijibu akiwa kasimama palepale mlangoni. Hakutetereka.

Akageuza shingo kutazama nyuma, akaiona. Akaiendea upesi na kutoka nje kwa kasi ya mwanga, "Nd'o hii?" alisema akiinua juujuu. Akamwaga vyote vilivyokuwamo ndani yake. Pesa, kioo, wanja na vikorokoro vingine vya kike vilikuwa wazi chini vikitapakaa ovyo mlangoni. Akatupa jicho lake na kusaili kila kimoja. Akachutama na kuchukua pesa zilikuwa kama elfu arobaini na kitu. Akazisunda kibindoni, mama hakuweza kumfanya kitu. Hakuwa tena katika ari ya kupambana na mtu yeyote. Yaliyomtokea yalimtosha.

"Haya okota uchafu wako upesi kabla sijafungulia kipigo kingine," alisema binti huyo akionesha chini kidole chake cha shahada aokote vitu vyake. "Changamka!" alifoka akimtolea mfano ainame chini kuokota vitu vyake. Kauli hiyo ya ukali ikamshtuka sana mama huyo, hakuwa sawa. Hakuna hata kimoja alichoamini kama kimemtokea. Tena katika siku ya kwanza ya uhuru wake.

Akainama kuokota vitu vyake huku chozi likimtoka. "Hili unalonifanyia utakujalipia!" mama huyo alisema akimaanisha kwa kile alichokisema. Akiwa katika kufikia vitu vya mbali kiasi, binti akaiwahi pochi, akaishika, akainua kichwa kumtazama yule mama aliyekuwa akiokota vitu vyake.

"Hii yaani nayo inaitwa pochi?" alisema akiinua juu kwa dharau huku midomo akiibetua—mkono wa kuume kiunoni. Akarudi ndani kwa kasi mithili ya kichaa, akatoka na kisu. Akakiinua juu kama anataka kumchoma nacho, badala yake akaishi kuitoboa pochi ya mama wa watu pasi na kufikiria anayemfanyia vile ni mwanamke mwezake tena mwenye umri uliopitia mengi. Mama yule alibaki akimtazama na asiwe la kufanya.

"Dunia ushanifunza tayari. Mafunzo yako yanatosha mimi kuwa na subira!" akainamisha kichwa chini akitazama vitu alivyovikota, akatikisa kichwa kisha akavifungasha katika khanga yake kama kifurushi. Akainuka na kuianza safari akiwa anachechemea. Hakufika mbali, bodaboda ikapita, akaisimamisha.

"Naomba unipeleke Tabata Aroma," mama alisema akipanda bodaboda ile. Damu ziliendelea kutoka kidogokidogo.

***

## MLANGO WA PILI

MJI ulikuwa umepoa kupita maelezo, si uani wala barazani kote kulikuwa kimya kabisa.  Milango yote ilikuwa imefungwa, dalili kamili ya kwamba wenyeji bado hawajaamka. Bodaboda ilifika hadi barazani, kwao napo ni kama kwake tu. Hakukuwa na mabadiliko yoyote yale. Angalau kwake alikuta mtu tofauti na mumewe wala wanawe.

"Kiasi gani malipo?" mama aliuliza.

"Elfu moja tu, mama!" bodaboda alijibu.

Akafungua fundo la khanga yake upande mwingine, aliiweka hii pesa kama bahati tu hakufikiria kama yangetokea yaliyotokea. "Ahsante, baba!" mama alijibu. Bodaboda akaondoka zake, akabaki peke yake kasimama mbele ya nyumba yao. Mazingira ya nyumbani mbali na kule kulikokuwa kwake wala gerezani. Mawazo mapya tena, akilini alikuwa akiwaza pengine yatamfika mengine mbali na yale aliyoyapitia huko alikotoka.

"Haiwezekani!" mama alijibu akielekea mlangoni. Akagonga mlangoni kwa nguvu. Hakutoa sauti. Kimyakimya aligonga mara tatu mfululizo.

"Naaaaniiii huyooooo jamani eeeeh!" sauti kutoka ndani ilipiga yowe la kughadhibika na ugongaji. Kwa mbali alisikia miguu ikitembea kuja upande wa mlangoni, akajiweka sawa kwa lolote lile. "Dunia na

mji umebadilika! Nikae tu sawa kwa lolote lile," alijisemea nafsini wakati huo hatua hizo zilifika kabisa mlangoni. Kadiri harakati za mlango kufunguliwa zilivyokuwa zikizidi, ndivyo mapigo ya moyo wake yalivyosonga kasi kwa hofu na wasiwasi wa atakayekuja kuufungua huo mlango.

Hakuamini macho yake.

Akapiga magoti chini kwa kuomba Mungu kwa kile alichokiona. Chozi la uchungu likaanza safari ya ahadi ya kutoka pindi nyakati za huzuni uliochanganyika furaha zikitokea. Alikuwa binti yake aliyesimama mlangoni. Safari hii akiwa mwanamama kabisa. Msichana mwenye umri kati ya miaka ishirini na moja kuelekea ishirini na mbili.

"Mama!" alitoa sauti kubwa sana.

"Sabrina, mwanangu!" aliitikia akimkumbatia mwanawe. "Mwanangu jamani! Uwiii!" mama Sabrina aliendelea kulia kwa furaha. Akatoa kumbato lisilomithilika. "Nilijua nitakufa kabla ya kukuona tena mwanangu. Jamani mwanangu!" alizidi kulombokeza. Sabrina akajitoa maungoni kwa mamaye. "Ma' mdogo, ma' mkubwa! Bibi!" Sabrina aliita akirudi ndani mbio.

"Mama karudi! Mama karudi!"

"Nani *kobwela?*" bibi yake Sabrina alisema akijitahidi kuinuka mkekani sebuleni alipokuwa amejinyoosha. "Mama huyo. Bibi na wewe?" Sabrina alijibu akifurahi. Mama Sabrina hata kuinua mguu kuingia ndani alishindwa. Alizidiwa na furaha pamoja na mshangazo wa kwa mumewe. Mambo yalikuwa tofauti sana. Mapokezi ya awali hayakumpa hamasa ya kuwa na furaha kubwa kabla ya kukutana na rangi halisi ya dunia.

"Mama! Mama njoo ndani huku sebuleni!"

Akajitoma ndani kwa hadhari kubwa. Ndugu wengine wakawa wanatokea vyumbani mwao wakakutana na dada yao koridoni. Zikalipuka kelele za furaha kubwa mno. Wakamkumbatia kila mmoja

kwa uwezo wake. Hakuwa na la kusema. Walivyomaliza furaha zao, mama Sabrina aliyekuwa akilia muda wote, wakampa fursa ya kupata hewa wakiwa kando naye. Akaketi mkekani alipokuwa mama yake mzazi, ambaye wakati huo alikuwa bubu wa ghafla. Ngozi ya mashavu ilimshuka na kulegea kupita kiasi. Paji linang'aa uzee. Hata macho yake yameacha usuhuba naye. Zaidi alitazama kwa kuvizia kumtambua aliyekuwa mbele yake. Vyote hatotambua lakini sio sauti ya mwanawe kipenzi. Mwanaye mwenye kuhangaika na kuilisha familia. Mtetezi na mpinga njaa wao.

"Mwanangu!" bibi yake Sabrina aliitaka huku akichuruzikwa na machozi. "Tulikususa mwanangu!" akaongeza. Mama Sabrina akajisotesha hadi karibu kabisa na mamaye, akamshika shavu la kulia. Akamfuta machozi, akaongeza ukaribu zaidi na kukiweka kichwa cha mamaye juu ya matiti yake. Akasema; "Usijali mama'ngu. Maneno yangu yalinifikisha kule nilipokuwa! Ulijaribu kunisihi sana juu ya maneno yangu lakini sikuwahipo kukusikiza. *Kila mchuma janga hulila mwenyewe kama wa kwao walitoa rai juu ya mwenendo wake*!"

Akajitoa kidogo huku akimrudisha nyuma mamaye ili kumtazama sura yake. "Hujazeeka sana mama'ngu. Basi tu vile miguu imeamua kukudhulumu mwendo!" aliongeza utani mama Sabrina. Mamaye hakuwa na la kusema. Furaha yake ilizidi yote yale aliyowahi kusema juu yake. Kuiona sura ya mwanawe ni kubwa kuliko chochote kile.

"Mwanangu!" bibi Sabrina alisema akitanua mikono ili akumbatiwe tena. Maana ile mara ya kwanza, haikutosha. Mama Sabrina akavunja goti na kumkumbatia mama'ke. "Imekuwaje tena? Mbona?" bibi Sabrina aliuliza akiwa katika mshangao mkubwa. Furaha ilivyoaga kuagana na mioyo yao, wakagundua kama ndugu yao ana majeraha. Wakachukua spirit na pamba, Mungu bariki ndani pia

walikuwa na dawa ya kuoshea vidonda hivyo walimsafisha damu zote na kuweka hali ya usafi katika maeneo yaliyopata athari za kipigo.

Wakataka kujua nini kilichotokea lakini hakutaka kuligusia hilo kwa sasa.

***

NDUGU wote wakakutana sebuleni kumpokea ndugu yao aliyetoka katika mdomo wa mamba kiajabuajabu. Hakuna hata mmoja aliyeamini kama kweli leo mama Sabrina yuko uraiani. Furaha zilikithiri ndani ya nyumba hiyo. Kutokana na kiu ya kutaka kujua maisha ya jela yapoje, akawasimulia kuanzia ile hali aliyopokelewa nayo tangu siku ya kwanza—vile hakuamini kilichotokea kama ni kweli ameishia katika shimo la kiza, tena bila kuwa na mwisho. Mchana wake aliofikishwa, mandhari ya ndani, watu waliompokea, masingi, manyanyaso na vitu vyote vinavyoweza kutia dhiki ya nafsi.

Siku ya kwanza, ya pili tatu nne hadi wiki. Mwezi ukafika hakuwa na wasiwasi tena kwamba gerezani ndipo mahali pake hadi anaingia kaburini. "Haikuwa rahisi hata kidogo ndugu zangu. Sio rahisi. Nilipofikisha miaka mitano, ile imani nilijianzishia ya nitakuwa hapa hadi kufa ndiyo ilikomaa zaidi. Japo huko nyuma mwanasheria wangu alinisihi sana niwe na nidhamu pengine nitapunguziwa adhabu. Hata katika suala la kukata rufaa nilimwambia ngoja kwanza sababu tu sikuwa tayari tena kupoteza mapesa kwa ajili ya kesi. Sikutaka niondoke niwaache wanangu wakiwa katika hali mbaya kiuchumi. Japo sielewi baadhi yao wako wapi!" alivyofikia kipengele hicho chozi likaanza kusafiria nyota ya huzuni wake.

"Basi tena, dada, jikaze!" mdogo'ake alimtuliza kidogo. "Ahsante, mdogo'angu," akajifuta chozi kidogo na khanga yake. "Maisha ya mle huoni nje ya ukuta ni mtihani kwa kweli. Haijawahi kupita siku bila kuwakumbuka ndugu zangu. Angalau dada ulikuwa ukija kuniona mara kwa mara," akaongeza. Kimya kikapita kwa

sekunde kadhaa, akasema; "Lakini mbona hukuwahi kuniambia kama wanangu hawaishi kwa baba yao wala hawako mahali pamoja?" akamwachia dadaye ajielezee.

Wakatazamana kwanza.

"Hichi sasa kimbembe!" dada mtu alijibu kwa sauti ya chini. Kila sura tena hapo ndani ikaanza kuangalia upande mwingine. Wakatia mughma cha nafsi ndugu yao. "Mbona kila mtu amebaki kimya, kulikoni?" aliuliza baada ya kuona hakuna majibu kabisa. Mamaye alibaki kama alivyomkuta hapo awali. Kuulizia habari za watoto nyuso zao zikasawijika.

"Yule bwana baada ya kuona umefungwa kifungo cha miaka thelathini jela, akaanza visa." akanyamaza kidogo kumeza funda la mate. Akaongeza; "Akaanza maisha mapya ya kujiachia na wanawake zake ndani ya nyumba yako. Kama haitoshi, akaoa kabisa mke wa kwanza. Tukaenda kuanzisha mbilinge…"

"Basi usiendelee!" mama Sabrina alidakia.

"Kwa nini sasa?"

"Yashapita hayo!"

Ndugu wakatazamana tena, hawakuelewa kwa nini ndugu yao hataki kusikia habari zile. "Hayatanisaidia chochote kile kwa sasa," akaongeza na kunyamaza. Akaendelea; "Haya majeraha nimeyapata hapohapo nyumbani kwangu. Nilipotoka jela tu, breki ya kwanza ilikuwa huko. Kilichonikuta ni udhalilishaji wa hali ya juu. Sikutaka historia ijirudie. Badala yake, nikakusanya virago na kurudi kwetu. '*Bora Uhai*' alisema *Ntila Vika wa Reading Marathon*—mengine yote ninaweza kuhaingaika nikayapata tena. Sikuwa tayari kuleta janga jipya nikarudi nilipotoka. Moyoni nilikuwa naomba Mungu kwa kila pigo nililopigwa nisirudishie maana najua mwishowe nitaonekana sijajifunza pamoja na kukaa ndani miaka kumi. Itoshe kusema

nimezaliwa upya!" alisema akijinyoosha. Ndugu hawakuwa na la kumweleza…

***

SIKU zilivyoenda, taarifa zilienea kwa ndugu zake kwamba mama Sabrina katoka jela. Alikuwa na ziara ndefu ya kutembelea ndugu jamaa na marafiki. Karibia mwezi mzima ulikuwa wa kutembelea watu aliokosa kuonana nao kwa kipindi kirefu. Pia hata ajabu ya kuchoropoka kabla ya wakati. Binafsi aliamini Mungu ana kusudio lake. Ndugu ama marafiki wengine walishindwa kumwona mama Sabrina akiingia na kutoka, hivyo walikaa naye kwa kipindi fulani kabla ya kwenda kwa ndugu mwingine.

Zaidi alikuwa akijaribu kuomba msaada wa kurudisha biashara zake za mama n'tilie ili ajikimu kimaisha. Hakutaka kuwa mzigo kwa mtu yeyote yule zaidi maisha ya kujibebesha kwa watu hayakuwa yake tangu hapo awali. Mizunguko ilivyoisha, chini ndugu na marafiki wakakaa, wakakubaliana.

"Kusema kweli ma' Sabrina kasaidia wengi sana. Ndiyo maana kuondoka kwake kulileta pengo kubwa sana. Hatuna budi kukubaliana na ombi lake tu jamani tumchangie apate japo cha kuanzia biashara zake," msemaji wa kwanza alisema katika kikao cha dharura kilichofanyika Kigogo Luhanga kwa ndugu wa mama Sabrina maarufu kama Binti Kimoto.

Kikao kikazaa matunda, baada ya muda fulani wa ahadi na wale waliotoa, mama Sabrina akapatiwa kiasi cha shilingi milioni moja na nusu, akarudi tena ofisini kwake kwa zamani na kukutana mabadiliko makubwa ya kiujenzi. "Loh! Nd'o mambo ya siku hizi mafuremu kila mahali eeh!" alisema akinong'ona mama Sabrina. Hakutaka mbali na pale pa zamani, ile nyumba aliyokuwa akifanyia biashara, imeuzwa. Imenunuliwa na mwuzaji vifaa vya ujenzi mkubwa eneo la Buguruni.

Bahati ilikuwa upande wake nyumba ya jirani ilibaki lakini maboresho ya fremu yalihusika.

Kulikuwa na kizimba kimoja kiko wazi, akalipia na kufanya marekebisho kadhaa ili kukidhi ofisi ya mama n'tilie. Akanunua vifaa vyote vinavyotakiwa katika ofisi yake, wiki moja mbele huku akiwa na vijana kadhaa aliowapata, kazi ilianza. Ni kama biashara nyingine tu, mwitiko haukuwa mzuri sana lakini aliendelea kujipa moyo. Hata usoni mwa watu wengi alikuwa mgeni kwao. Wale aliofahamiana nao walibaki wachache sana.

Polepole walianza kurudi wateja wake wa mwanzo, huduma ilizidi kueleweka. Awali asubuhi alikuwa akipika chai, maharage, chapati na maandazi. Vitumbua aliagiza kwa watu wengine.Baadaye akaongeza supu ya utumbo, akazidi ya nyama, samaki, na mwishowe ya kuku. Kijiwe kikapamba moto. Ubora wa mapishi yake ukapelekea kuongeza fremu ya pili ambayo pia ilikuwa haina mtu. Mwenye nyumba akakubali kutoboa mlango wa kuunganisha fremu zote mbili ili kurahisisha zoezi la huduma kwa wateja wake.

Moto ukawaka!

Salamu zikawafikia wahenga kwamba yule mchawi wa mapishi amerudi tena mjini. Mrindimo wa vyakula vyenye ladha umetanda Buguruni Ghana yote. Sasa oda za chakula zilianza kuenea maeneo mbalimbali. Hakufanya kazi kwa mazoea, ulichokula jana ndicho utakachokula leo. Ubora ni uleule. Ndani kukawa hakutoshi, ikamlazimu anunue viti na kuviweka nje ya fremu—Mungu bariki kulikuwa na miti kando hivyo haikuwa jambo gumu kuvipanga viti katika eneo hilo.

"Ahsante Mungu baba kwa kunirudisha tena mjini!" alisema mama Sabrina akiwa peke yake nyumbani kwake alipopanga maeneo yaleyale karibu na ofisi yake. Kitandani alikuwa akihesabu noti chungutele. "Nimerudi baba! Nimerudiii!" alisema akinong'ona. Moyo

wake ulijaa furaha tele. Hakutaka kujiaminisha kwamba alikuwa na uhakika na alichokuwa anakifanya bali imani na juhudi ya dhati imemfikisha alipotaka. Akiwa katika lindi la furaha, akashtushwa na mlango uliogongwa usiku huo.

Alivyotazama saa ya simu yake, ilikuwa tena inakaribia saa sita usiku. Ana masaa matatu ya kulala kabla ya kuamka saa tisa usiku kuelekea Vingunguguti machinjioni kuchukua nyama kwa ajili ya supu na vitoweo. "Nani tena huyo saa sita usiku wote huu?" alijiuliza huku akifunika vyema pesa zake alizozimwaga kitandani kote. Akainuka polepole hadi mlangoni. Akatafakari kiasi, akaazimia kuuliza aliyekuwa nje.

"Nani huyo?" aliuliza kwa sauti ya juu kiasi.

"Mi' hapa?"

Mtima wake ukapasuka paa! Sauti hiyo anaijua vyema. Ni sauti ambayo hakutaka kukutana nayo wala kusikia baada ya yale yaliyomfika pale nyumbani kwake. Hakutegemea kuisikia hivi karibuni. Imekuwaje? Nini kilichomleta? Alikuwa na maswali mengi yakishindana kichwani kwake. "Unasemaje?" angalau aliweza kuhoji dhamira ya kile kilichomleta. "Fungua mlango tuongee mama watoto!"

Nguvu zikamwishia. Akajikuta akirudi nyuma hadi kitandani, akaketi kwa kujipweteka pwee! Kijasho kilianza kusafiri kuanzia katika uti wa mgongo, hadi maeneo yote ya mbavu na mgongoni kote kwa ujumla. "Naomba tuongee tafadhali!" akaongeza. Safari hii sauti yake iliangiwa na huzuni kwa mbali. Akajizoazoa mama Sabrina hadi mlangoni, akatazama kitasa mara mbilimbili, akajitafakari aidha anachofanya ni sahihi au la. Akili yake ikarudi tena nyuma, hadi siku yake ya hukumu, siku ambayo maisha yake yalibadilika. Siku ambayo ilisabaisha atengane na familia yake kwa miaka kumi. Mume hakuja, wala hakutuma barua, wala hakumkumbuka kwa maji ya kunywa,

sabuni, hata salamu ya bure hakuwahi kupata kwa kipindi chote alichokuwa gerezani.

Akafikiria wanawe waliofukuzwa na kwenda kuishi na nduguze ilhali baba yao yu hai mzima mwenye siha njema. Basi tu aliamua kufanya hivyo kwa kuona kwamba hatarudi tena uraiani—atabaki ndani milele. Kuna sauti ikamwambia, '*huyo si binadamu!*' akajikuta akirudi tena kitandani, akaketi akiendelea kuwaza na kuwazua. Akatoa sauti.

"Nimechoka sana kwa leo naomba tuonane kesho!"

Akabaki akisikilizia ukimya hafifu uliotokea huko nje ya chumba chake.

"Sawa! Nimekuelewa!" bwana huyo aliitikia kinyonge, akaondoka. Hakuishia hapo, bwana huyo aliendelea kumsumbua kila siku ofisini kwake. Tangu ajue amerudi, hakuwahi kuiacha siku ipite bila kwenda mgahawani kwa mama Sabrina. Baada ya kero mbalimbali hatimaye kikatokea kisa cha usemi wa '*Atafutaye hachoki, hata akichoka, keshapata*!'

"Haya, niambie unasemaje. Maana umezidi kunifuatafuata!" mama Sabrina alisema kwa hamaki baada ya kukutana na mumewe wa zamani. Waliketi kando peke yao bila bughudha. "Wewe bado ni mke wangu!" bwana huyo alijitutumua. Akasababisha mbetuko wa papi za midomo ya mama Sabrina bila kutarajia. Akampandisha na kumshusha kwa wakati mmoja.

" Ati unasema?"

"Wewe bado u ngali mke wangu!"

"Kasema nani maneno hayo?"

"Mimi hapa!"

"Kumbe!"

"Ndiyo. Ina maana hujui au?"

Mama Sabrina akapitisha kimya kwa nukta chache, akashusha pumzi akamsaili bwana kama huyo aliyekosa haya hata punje kwa kwenda ofisini kwake na kutaka kujipa umume ulioyeyuka miaka tele nyuma. Tena yeye ndiye aliyekataa mke kwa kutoenda kumuona akiwa gerezani. Akamtazama kwa chati kisha akamwuliza;

"Kipi hasa kitakachonifanya nirudiane na wewe?"

"Hilo tu?"

"Dogo hilo?"

Kukapita tena kimya cha kutegana kwa nukta chache, kwa kujitutumua akajibu, "Watoto!" akarudisha sura yake upesi machoni kwa mama Sabrina kutazama tokeo la jibu lake. "Ha ha ha ha ha!" mama Sabrina alicheka kwa dharau. Akacheka na kucheka hasa kicheko cha dharau kilichobebeshwa ngata ya 'unikome!' Alivyomaliza, akamgeukia kwa kinyodo hasa, akamwuliza.

"Wako wapi hao watoto?"

Bwana tena akaingiwa na baridi. Yumkini hakutarajia kutupiwa swali kama hilo katika kipindi ambacho alijiona hawezi kupingwa kwa kile alichokuwa akiamini anapendwa na huyo mwanamama. Akajishika kichwa, sura akageuzia upande mwingine, mara akageuka nyuma kutazama kama watu walikuwa wakiwazingatia ama la. Hasha. Haikuwa hivyo. Kila mja alifanya lake.

"Achilia mbali hilo," mama Sabrina akaongeza. "Kwa nini hukuwahi kuja kunitembelea gerezani hata siku moja? Nd'o ahsante ya kukupenda hiyo?" akahitimisha swali lake. Akamwacha baba Sabrina ajing'ateng'ate mwenyewe. "Nakusikiliza!" mama Sabrina alihimiza jibu lake. Kimya kikatanda katika ubongo wa baba Sabrina. Mama Sabrina alivyoona mzee mwenzake hana majibu, akamjibia.

"Ulikuwa na wazo gani kwani?"

"Nilitaka turudiane mke wangu!"

"Hilo tu?"

"Ndiyo, mama Sabri!"

"Njoo kwetu uongee na familia yangu..."

"Sawa—nitakuja!"

***

NYUMBANI kwa baba Sabrina akiwa na banati mpya aliyemwoa hivi karibuni, jioni moja iliyotakasika mioyoni mwa wapendanao hao walijikusanya sebuleni wakitazama vipindi mbalimbali vya runinga huku miguu juu ya meza. Maisha wameyakatia denge kama wasemavyo vijana. Mume alileta hadithi za maisha ya ujahilia wake, jinsi alivyokuwa chakaramu kila kukicha. Namna alivyokuwa akibadili wasichana kama njugu. Vicheko mpaka jino la mwisho kwa kuhadithia yaliyosibu usuli wa maisha yao.

"Basi bwana siku kadhaa kama si miezi huko nyuma, alikuja mwanamke mmoja kujitia wazimu hapa, aisee!" mke wa baba Sabrina alianzisha maongezi akicheka. "Mwanamke gani tena? Alikuwa anataka nini?" baba Sabrina alihoji akitoa macho. "Nilimtandika na mkanda kama mtoto wa kumzaa mwenyewe!" mke huyo aliongeza.

"He! Mbona hukuniambia hiyo stori?"

"Ah, si nimefuata yale maneno yako kama atatokea mtu anazingua kuhusu mjengo nitembeze kichapo? Sijanyeka mie ati!" akaongeza jibu la kifidhuli. Baba Sabrin a akili ikamcheza. Ikabidi ainuke akae kitako kwa umakini zaidi ili aweze kuelewa kiini cha kutandikwa mikanda huyo mwanamke aliyesema kaja kishari kuhusu nyumba.

"Kwani alisemaje?" baba Sabrina alihoji akitweta. Kwa fahari kubwa binti huyo akasema; "Ati anadai yeye nd'o mwenye nyumba hii na wale watoto waliokuwa katika picha ya ukutani ni wanawe!" akasindikiza na dhoruba la cheko lililomshitua baba Sabrina. Akili yake ikavamiwa na hofu mithili ya mtu aliyekutana na simba ama chui mtaka

roho ya mwanadamu. Akaingiwa na wahaka, ukajibanza katika kila kona ya mishipa ya fahamu yake.

"Atakuwa mama Sabrina huyo!" aliwaza nafsini bila kupiga kelele. "Atakuwa katoka lini? Haiwezekani…. Mbona miaka thelathini bado?" kiti kikawa cha moto ghafla. Akamtazama mkewe wa sasa kwa jicho la hadhari. Kitumbua kimeingia mchanga. Akili haimpi. "Vipi tena mume wangu mbona kama vile umeona mzuka?" mke wake aliuliza kwa wasiwasi baada ya kumuona mumewe akitambaliwa na mshikemshike wa wasiwasi usoni. Usowe ulibadilika ghafla.

"Kwani ni kweli aliyoyasema yule mwanamke?" mke aliuliza huku akizidi kumakinika. Moyoni alijua jibu litakuwa ndiyo, akajipa ujasiri wa mshumaa kumulikia wenzake huku yeye akiteketea. Mume akajibaraguza—hatimaye akakubali kwamba yule aliwahi kuwa mkewe. Ikamlazimu kumwelezea mkasa wa uwongo ili kumficha mke mpya.

"Kwa nini hukuniambia siku zote hizo?" mume alihoji baada ya kueleza kisa cha uwongo kumuhusu mkewe wa zamani.

"Niliona haina maana. Nilimchukulia kama chizi fulani tu!"

"Doh! Ulikosea sana!"

"Kwa nini sasa? Si nilifuata maelekezo yako au umeyasahau?" mke alijibu kwa hasira. Mume akatulia kiasi. Wakayasema yakaisha. Mume akaanza safari za kufuatilia rasmi nyayo za mkewe wa zamani. Hakuthubutu kwenda nyumbani kwa mkewe kuhoji ilikuwaje kwa hofu ya kufurushwa. Alianza kwenda kwa mashoga wa mama Sabrina kwanza kujua kama alichokisema mke wake wa sasa ni kweli ama la? Karibia kote hakupata majibu mazuri lakini kuna mmoja alikuwa akielewana naye sana. Na ndiye aliyemkuwadia wakawa wapenzi kitambo hicho. Huyu hakuleta vurugu sana japo hakupendezewa na tabia ya baba Sabrina.

"Umezingua sana. Huwezi kumwacha mkeo asote gerezani bila kwenda kumwona na ukafukuza watoto wake," alisema upesiupesi mwanamke huyo aliyekuwa akinywa chai huku anaongea. "Tena sana! Sana mno! Wewe sio mtu kabisa. Hawezi kubali mrudiane. Ohooo mi' nd'o nakwambia sasa!" akameza funda la chai, akatoa mboli kiasi akiiziba na kiganja cha mkono wake wa kulia. Akatoa tabasamu, sura upande wa baba Sabrina. Lile la dharau kabisa kwa kutomwelewa baba Sabrina.

"Nikusaidieje?" aliuliza akitulia sasa mama huyo.

"Niambie anaishi wapi."

"Siwezi kukwambia."

"Kwa nini sasa?"

"Hana mpango na wewe. Hataki matatizo mengine tena!"

"Lakini wewe hilo si jukumu lako..."

"Nd'o hangaika mwenyewe ujue anaishi wapi!"

Bwana akaghadhibika. Alipogtegemea angepata msaada, hakuupata. Akaanza kuzurura ovyo kila mahali—hata akili ilivyompa arudi tena ofisini kwake kwa zamani, pengine atapata mwangaza. Kumbe nd'o alikuwa anaenda kukutana naye uso kwa macho. Akiwa anakaribia ofisini kwa mama Sabrina, akajibanza katika kichochoro kutazama mazingira. Alikuwa makini mithili ya askari mpelelezi anayemfuatilia mhalifu katika mihanjo yake. Haichukua muda, mama Sabrina akawa anapita na vifaa vyake ya kazi, sahani na chupa za soda akirudi ofisini kwake. Akaendelea kumtazama ataishia wapi.

Zaidi alijua ofisi yake ya zamani ilivunjwa kutokana na maboresha usasa lakini hakutegemea kama angerudi tena eneo lilelile kuja kufanya kazi ileile. Aliendelea kuchunguza hadi alipoishia ni jengo la pili baada ya ile ofisi yake ya zamani. Akashusha pumzi. Mama Sabrina alipiga harakati zake akiwa hana habari kama kuna jicho la mtu linamchunguza nyendo zake. Baba Sabrina aliendelea kuja mara kadhaa

hadi hapo alipopoata wazo la kumfuatilia nyumanyuma mama Sabrina hadi nyumbani.

"Duh! Mwanamke ana mambo mengi huyu hata akifika nyumbani atakuwa hoi," alijisemesha mwenyewe baba Sabrina. Alitoka ofisini akapitia madukani kwanza kulipa pesa ya vitu alivyochukua asubuhi, akazunguka sehemu mbalimbali hadi anafika kwake ilikuwa inakaribia saa sita usiku. Baba Sabrina bado alikuwa akijiweka mbali naye ili ajue ataishia wapi. Hatimaye alifika katika nyumba aliyopanga mama Sabrina.

Akazidisha umakini kwa kutazama ni mlango upi ataingia mkewe wa zamani. Nyumba ilijengwa mtindo mithili ya garimoshi. Ndefu ikiwa na vyumba vitano kila kimoja kinajitegemea. Usoni pake hakuna kitu zaidi ya kisima na shimo la taka ambalo lilichimbwa kwa minajili ya kuchukua mchanga uliotumika kujengea choo cha nyumba hiyo. Sasa wapangaji wanatupia taka zao humo ili kulifukia. Mama Sabrina aliingia chumba cha kati, kati ya viwili kulia na viwili kushoto. Pazia lake la rangi nyekundu iliyopauka iliyochanganywa na vimaua vya rangi nyeupe. Kwa hadhari kubwa ukizingatia usiku ulikuwa mkubwa, akasogea na kugonga.

***

"NILIJUA tu asingekubali kunifungulia!" alijilaumu baba Sabrina. "Hata hivyo si mbaya—angalau nimejaribu!" akaongeza. Hakuishia hapo, aliendelea kumsumbua mkewe huyo wa zamani hadi alipokubali kuweka naye mazungumzo ya kurejesha pendo lao kama lilivyokuwa.